# Nuhu




Mungu alipomuumba binadamu, alimuumba kwa mfano wake mwenyewe.
Nao walikuwa mume na mke.
Mungu akawabariki na kuwaita “Mtu.”
Baada ya kuishi kwa miaka 130 Adamu alimpata mwana mwenye kumfanana, naye akamwita Sethi.
Hawa mkewe akawazaa watoto wengine baadaye, wa kiume na wa kike.
Sethi akamzaa Enoshi.
Enoshi akamzaa Kenani.
Naye Kenan, Mahalaleli.
Mahalaleli naye akamzaa Yaredi.
Yaredi naye akamzaa Henoko.
Henoko alikuwa babaye Methusela.
Henoko alitembea katika njia zake Mungu, na kummpendeza, hadi Mungu akamleta mbinguni.
Methusela alimzaa Lameki.

Naye Lameki alikuwa na mwana aliyemwita Nuhu.

Lameki akinena, “Huyu ndiye atakayetufariji kwa kazi yetu na kwa taabu ya mikono yetu katika nchi aliyoilaani Bwana.”
Nuhu akawazaa Shemu, na Hamu, na Yafethi.

Nuhu, maana yake ni faraja.




MWANZO 5:1-32



Mungu akaanza kuongeza idadi ya watu duniani na kuwapa kipimo cha miaka 120.
Mungu akaouona uovu wa binadamu na kungámua kuwa daima moyo wake unapanga maovu.
Mungu akasema, “Nitawaangamiza watu niliowaumba pamoja na kila kiumbe kinachotambaa ardhini, n ahata ndege wa angani kwa maana nasikitika sana kwa kuwaumba”.
Lakini Nuhu alipata kibali machoni pa Mungu.
Hii ndio hadithi yake Nuhu.
Nuhu alikuwa mnyoofu na mwenye haki katika jamuia ya watu alikoishi naye alimfwata Mungu kwa moyo wake wote.
Nuhu na mkewe walikuwa na watoto watatu - Shemu, na Hamu, na Yafethi
Mungu akamwambia Nuhu…
Nimeamua kuwaangamiza binadamu wote; kwa maana duniani kumejaa jinai. Naam, nitawaangamiza binadamu wote duniani.
Jenga safina ya mti wa mvinje; fanya na vyumba ndani ya safina, ukaifunike ndani na nje kwa lami. 15 Iwe na urefu wa futi 450, upana wa futi 75 na kimo cha futi 45.
Utengeneza dirisha la kuizunguka safina na liwe nchi kumi na nane chini ya paa; ukaifanyie dari tatu, ya chini, ya pili, na ya tatu na ukautie mlango wa safina katika ubavu wake
Tazama nitaighubika nchi kwa gharika na kukiangamiza kila kiumbe cheenye uhai
-kilachenye kniachopumua.
Lakini, ninakuahidi ya kuwa utakuwa salama ndani ya safina, wewe, mkeo, wanao na wake zao.
MWANZO 6:1-22



Mungu akampa Nuhu maagizo…
"Uwalete kila aina ya mnyama – wa kiume na wa kike katika safina ili wahifadhiwe dhidi ya gharika. Vile vile kwa ndege wa angani na chochote ktambaacho."
"Uwahifadhi katika safina pamoja na chakula ambacho mtahitaji."
Nuhu alifanya kila kitu jinsi alivyoamuriwa na Mungu, nao wakaingia katika safina.
Siku saba baadaye…
MWANZO 6:19-7:10


Hiyo siku chemichemi zote zilitoa maji na kufurika, nayo malango ya mbingini yakafunguliwa. Nayo mvua ikanyesha duniani kwa siku arobaini, usiku na mchana.
Kwa kipindi cha siku arobaini mafuriko ya dharuba kali yaliifunika nchi huku safina ikielea juu ya maji. Maji yalivyozidi kupanda, ndivyo safina ilivyozidi kuelea ju ya maji; hatimaye milima yote chini ya mbingu ikawa imefunikwa na maji.
Vitu vyote vyenye uhai vikaangamia- ndege woe, wanyama wa nyumbani na hata wa porini, wenye kutambaa n ahata wa kuruka- kila kitu chenye pumzi kilichoishi katika nchi kavu.
KOOM
Kila chenye uhai juu ya nchi kiliangamizwa. Ni Nuhu tu na jamii yake na wale waliokuwa naye katika safina waliohifadhiwa.
Naye Mungu akamkumbuka Nuhu na wote waliokuwa nye katika safina akavumisha upepo juu ya nchi na maji yakapungua.
Genesis 7:11- 24


SAFINA ILITUA KATIKA NCHI KAVU KWA SIKU 150 NDIPO NUHU AKAMTOA KUNGURU.
MBONA UKAFANYA HIVYO BABA?
AKIWA KATIKA NYANJA ZA JUU, KUNGURU ANAO UWEZO WA KUONA NCHI KAVU. AKIREJEA, TUTAJUA KWAMBA MAJI HAYAJADIDIMIA-
LA, BABA, NI HIVI, KWA NINI ULIMTUMA KUNGURU MMOJA? TUNAO KUNGURU WAWILI TU. JE ITAKUWAJE AKIPATWA NA MABAYA?
WAKATI UJAO NITAMTOA NJIWA. TUNAO NJIWA SABA..
LAKINI NJIWA HAKUPATA MAHALI PA KUTUA KWA MAANA MAJI YALIKUWA MENGI.
JUMA MOJA BAADAYE…
KWA NINI KAKA, BABA?
ULIMTUMA NJIWA JUMA LILILOPITA NA HIYO HAIJALETA JIBU LOLOTE.
NDIO, NINA HAJA SANA YA KUJUA JINSI MAMBO YALIVYO KULE NCHE, LAKINI NAOGOPA KUUFUN-GUA MLANGO!
MWANZO 8:6-9


JUMA LINGINE
JE BABA WAONAJE, HUU NDIO WAKATI UNAOFAA?
HIVI KARIBUNI. NAJUA HIVYO.
TAZAMA, HUYO, YUAJA.
NDIO, BABA, ANARUDI! LAKINI ANA KITU MDOMONI!!!
JANI LA MZEITUNI!
JANI LA MZEITUNI!
NUHU AKAKAWIA JUMA LINGINE MOJA, HALAFU…
LEO, NAHISI KWAMBA HUYU NJIWA HATARUDI!
NINA UHAKIKA! HUYO NDEGE AMEPATA PUMZIKO!
BADO TUNA KIPINDI KIREFU CHA KUSUBIRI, NAONA HIVYO, KABLA YA NCHI KUKAUKA VYEMA, LAKINI-
--HAIJALISHI SANA HATA TUKISUBIRI KWA KIPINDI KIREFU, SIO KAMA TULIVYOSUBIRI WAKATI WA UJENZI WA HII SAFINA, BABA!
MWANZO 8:10-12


SIKU MIA TATU SABINI NA SITA BAADA YA BWANA KUIFUNGA SAFINA.
WANANGU, WAKATI UMEWADIA
LEO NDIO SIKU YA KUTAMBUA IWAPO NCHI IKO TAYARI KUTUPOKEA!
MIMI NIMEJITAYARISHA!
LO! NUHU!
TAZAMA!!!
...NCHI ILIKUWA TAMBARARE NA IMEKAUKA.
NDIPO MUNGU AKASEMA:
TOKENI NCHE, WEWE NA MKEO, WANAO NA WAKE ZAO.
MWANZO 8:14-15




MWANZO 8:17-19


WANANGU!
KUSANYENI MMOJA WA KILA MNYAMA MSAFI!
KWA NINI, BABA?
WATATOLEWA KWA MUNGU WETU KAMA DHABIHU.
SASA, MOTO
NJIWA, BABA.


ZAENI, MKAONGEZEKE KWA IDADI NA MUUJAZE ULIMWENGU.
MTUKUWA WAKUOGOFYA, WANYAMA WOTE NCHINI, NDEGE WA ANGANI, KILA KIUMBE KINACHOTAMBAA NA HATA SAMAKI WA MAJINI, WATAWAOGOPENI.
KWA MAANA WAMEWEKWA MIKONONI MWENU.
KILA KITU KINACHOISHI NA KWENDA KITAKUWA CHAKULA KWENU.
JINSI NILIVYOWAPENI MIMEA, HATA SASA NAWAPA KILA KITU.
LAKINI KWA UHAI WA DAMU KWA KWELI NITAHITAJI HESABU/MAELEZO.
NITAMWITAJI KILA MNYAMA AJIELEZE.
KUTOKA KWA KILA MTU PIA, NITAHITAJI MAELEZO KUHUSU UZIMA WA MWENZIE.
YEYOTE ATAKAYEMWAGA DAMU YA MTU, YAKE PIA ITAMWAG-WA NA WATU; KWA MAANA MUNGU AMEWAUMBA KWA MFANO WAKE.
LAKINI, ZAENI MATUNDA NA MUONGEZEKE DUNIANI.


NIMEUWEKA UPINDE WANGU MAWINGUNI, NA UTAKUWA ISHARA YA AGANO KATI YANGU NA NCHI.
NINAPOYALETA MAWINGU JU YA NCHI HALAFU UPINDE UONEKANE MAWINGUNI, NITALIKUMBUKA AGANO KATI YANGU NA WEWE NA VIUMBE WOTE WENYE UHAI:
HAITAWAHI FANYIKA TENA, YA KWAMBA MAJI YATAKUWA GHARIKA ILI KUANGAMIZA VYOTE VILIVYO HAI.
WAKATI WOWOTE UPINDE UNAPOONEKANA MAWINGUNI, NITAUONA KULIKUMBUKA AGANO LA MILELE KATI YA MUNGU NA VIUMBE WOTE WA KILA AINA DUNIANI.


NUHU NA JAMII YAKE KUANZA KAZI
KUILIMA NCHI.
KUJENGA MANYUMBA
KUWALINDA WANYAMA.
KUTENGENEZA MAISHA YAO MAPYA.
NI HISIA NZURI KUJENGA KITU CHA KUISHA BAADA YA SIKU MOJA AMA MBILI. EEH, AU SIO MANDUGU?
AFADHALI KUJENGA MJENGO USIOHITAJI KUPANDA NGAZI YA FUTI AROBAINI KWENDA JUU!
LAKINI HEBU FIKIRIA, SABABU KUBWA YA KULIJENGA HEMA HILI, NA SABABU KUBWA YA KUIJENGA SAFINA NI MOJA: TUSILOWE MAJI!
NA NUHU AKAPANDA BUSTANI.
BAADA YA KUNYWA DIVAI, AKALEWA.
MMM
NZURI. TAMU.


BABA?
MAMA ALIKUWA ANA---
OH, BABA!
NITAMANI YA KUWA HAWA NDEGE WANGALIKAWIA HAPA.
WALIONEKANA WENYE NYAMA NZURI, LAKINI WALIONDOKA NA PAMOJA NA WANYAMA WENGINE.
HAMU, KUNA NINI?
MWUULIZE BABA!
INAONEKANA, BUSTANI ALIYOIPANDA IMEOTA MAZAO, NA MZEE AMELEWESHWA NAYO.
HIVI SASA AMELALA KATIKA HEMA LAKE, UCHI JINSI ALIVYOZALIWA.
ENDENI MKAJIONEE!

MWANZO 9:22


NDUGU NMESHINDA NIKITAFAKARI, ILIKUWAJE BAADA ADAMU NA HAWA KUTENDA DHAMBI, JAMBO LA KWANZA WAO KUTAMBUA NI KWAMBA WALIKUWA UCHI.
LAKINI BABA…NI YEYE PEKEE YAKE ALIYEKUWA MNYOOFU KATIKA KIZAZI CHAO!
ALIYETEULIWA KWA WADHFA WA KUWAHIFADHI WANADAMU KUTOKANA NA MAOVU YALIYOMHUZUNISHA MUNGU!
KAKA NAKWAMBIA, WATENDA DHAMBI WENGI WAMEKWENDA, LAKINI SIO DHAMBI YENYEWE.
BADO TUKO HAI.
YAFETI, USIMWANGALIE.
HATUFAI KUIONA AIBU YAKE.
NI—NI NINI KILITENDEKA? MBONA NIMEFUNIKWA NA NGUO YAKE SHEMU
NUHU, ULILEWA DIVAI. UKAANGUKA HAPA,UCHI.
WANAO WALIKUONA —HAMU ALIKUONA UCHI, AKAONDOKA KWA DHARAU, LAKINI WANAO WAWILI WAKAAMUA KUKUFUNIKA.
HAMU? HAMU? ALAANIWE KWA KUNIACHA UCHI!
NA MUNGU AWABARIKI SHEMU NA YAFETI KWA KUNISAIDIA.
HAMU NA AWE CHINI YA WALIO CHINI! MUNGU AWAINUE WALE WENGINE WAWILI.
NUHU, SIO HAMU ALIYEIWEKA CHUPA YA POMBE MKONONI MWAKO.
WALA HAKUKUFANYA ULEWE HADI UJISAHAU. SIYE HAMU ALIYEKUTOA NGUO.
BAADA YA YOTE TULIYOPITIA, TAYARIMIMI NA MWANANGU TUMEINGIA KATIKA MAKOSA!
MWANZO 9:23-27




MWANZO 9:19, 28